



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MAOMBI YA USAJILI WA UWAKALA BINAFSI WA HUDUMA ZA AJIRA KWA**  
**MWAKA 2024/2025**

1. Kwa kuzingatia Sheria ya Kukuza Huduma za Ajira Na. 9 ya Mwaka 1999 na Kanuni zake za Mwaka 2014, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inapenda kuutangazia Umma kuwa, kuanzia tarehe 1 Juni, 2024 itaanza kupokea maombi ya usajili wa Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira. Aidha, usajili utatolewa kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe 1 Julai 2024 hadi 30 Juni, 2025.
2. Kwa mujibu wa Sheria tajwa Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira wamepewa jukumu la kuunganisha watafuta kazi na waajiri ndani na nje ya nchi pasipo kuwa sehemu ya mahusiano ya kiajira yanayoingiwa baina ya watafuta kazi na waajiri pamoja na kutoa huduma zingine zinazohusiana na utafutaji kazi kama vile kutoa ushauri na taarifa kuhusu soko la Ajira kwa watafuta kazi na waajiri.
3. Maombi ya usajili yawasilishwe kwa Fomu Maalum iliyowekwa kwa mujibu wa Sheria yakiambatana na nyaraka zifuatazo: -
  - i. Katiba ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Kampuni (**Memorandum & Articles of Association**);
  - ii. Hati ya Usajili wa Kampuni (**Certificate of Incorporation**) AU Hati ya Usajili wa Jina la Biashara (**Business Name**);
  - iii. Leseni ya Biashara (**Business License**);
  - iv. Namba ya Usajili wa Mlipa Kodi (**Tax Identification Number**);
  - v. Wasifu wa Kampuni pamoja na ujuzi na uzoefu wa wataalam katika uendeshaji wa huduma za Ajira (**Company Profile**).
  - vi. Uthibitisho wa Kampuni au Wakala katika kulipa kodi (**The Current Tax Clearance Certificate**);
  - vii. Anuani Kamili ya Ofisi (**Physical Address**);
  - viii. Mkataba wa Pango la Ofisi au Hati ya Umiliki wa nyumba inayotumika kwa Ofisi;

- ix. Hati ya tabia njema (**Police Clearance Certificate**);
- x. Taarifa ya utendaji kazi wa Kampuni ya Mwaka 2023/2024 (**kwa Wanaohuisha Leseni**);
- xi. Vyeti vya Taaluma (**Mtaalam wa Rasilimali watu**)

**Nyaraka zote ziwe zimethibitishwa na Wakili, Hakimu au Mamlaka iliyotoa nyaraka husika** (Kwa Nyaraka ambazo si halisi).

4. Maombi yawasilishwe kupitia Anwani ifuatayo: -

**Kamishna wa Kazi,  
Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu,  
S.L.P 2890,  
DODOMA.**

5. Maombi yaambatane na ada ya usajili ya kiasi cha **Tshs 500,000/=.**
6. Kwa maelezo zaidi Waombaji wanaweza kuwasiliana na **Emmanuel Nathaniel** kupitia Namba ya Simu **0715623320.**

Imetolewa na;

Kamishna wa Kazi  
Ofisi ya Waziri Mkuu  
Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu  
27 Mei, 2024.